**10 Septemba, 2024**

**TAARIFA KWA UMMA**

**TAMKO LA KULAANI UTEKAJI NA MAUAJI YA KIKATILI YANAYOTOKEA NCHINI**

Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kinasikitishwa na kinalaani kitendo cha utekaji na kuuawa kikatili kwa ndugu Ali Mohamed Kibao.

TLS, inapenda kuvikumbusha vyombo vya dola juu ya majukumu yake ya Kikatiba na Kisheria ya kulinda watu na mali zao. Haki ya kuishi na kulindwa kwa kila Mwananchi ni haki iliyoelezwa kwenye Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, kumekuwa na ongezeko la watu kutekwa na hatimae baadae kupatikana wameuawa kitu ambacho ni kinyume na katiba ya nchi yetu na ni kinyume na Mikataba ya Kimataifa kama vile **Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu** (Universal Declaration of Human Rights). Mnamo tarehe 6/9/2024 TLS ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa kupitia kwenye vyombo mbalimbali vya habari kwamba, usiku wa kuamkia tarehe tajwa mwanamke aliejulikana kwa jina la **Mwamvita Mwakibasa,** pamoja na mtoto aliejulikana kwa jina la **Salma Ramadhan** waliuwawa kikatili kwenye eneo la Kata ya Mkonze Jijini Dodoma. Mnamo tarehe 08/9/2024 TLS pia ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya mauaji ya kikatili yaliyofanywa dhidi ya **Ndugu Ali Mohamed Kibao.**

TLS kwa mamlaka iliyopewa kupitia **kifungu cha 4** cha Sheria iliyounda TLS (Tanganyika Law Society Act, Cap. 307 R.E. 2002), inatoa wito kwa Serikali na Taasisi nyingine kama ifuatavyo:

1. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan kuunda tume huru itakayochunguza matukio ya kupotea, kutekwa na kuuawa kwa wananchi ili kupata suluhu ya kudumu kwa lengo la kurejesha imani ya wananchi juu ya uhuru wao na haki za msingi za Kikatiba ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi ambayo sasa iko mashakani;
2. Waziri mwenye dhamana (Waziri wa Mambo ya Ndani), IGP pamoja na Mkuu wa mafunzo wa Jeshi la Polisi wawajibike;

3. Jeshi la Polisi lihakikishe kwamba linatoa taarifa sahihi kwa umma dhidi ya watu wote waliochukuliwa na kutekwa kinyume na sheria kwa kueleza taratibu walizochukua mpaka sasa kwa lengo la kuhakikisha watu hao wanapatikana;
4. IGP atoe tamko la kuvunjwa kwa vikosi kazi vyote vilivyoundwa ambavyo vimekuwa vikifanya kazi kinyume na sheria za nchi na kuelekeza kwamba, ukamataji wowote kabla ya kufanyika lazima awepo kiongozi wa Serikali ya Mtaa husika na vivyo hivyo wawe wanatoa taarifa kwa umma ya kituo cha Polisi alickopelekwa mtuhumiwa;
5. TLS imeona kuwa ziko sheria zilizopitishwa na Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zinatoa mianya kwa vikundi, taasisi au watu fulani kufanya kazi zao bila kuzingatia misingi ya haki nchini. TLS inapitia sheria hizo, na itazifikisha mahakamani kuzipinga kwa mujibu wa sheria na Katiba; na
6. TLS inavitaka vyombo vyote vya Dola Nchini kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi.

TLS inatoa pole kwa familia ya **Mwamvita Mwakibasa, Salma Ramadhan** na Ndugu **Ali Mohamed Kibao** kwa vifo vya wapendwa wao, pamoja na Chama cha Demokrasia na Maendeleo kwa kifo cha ndugu **Ali Mohamed Kibao.**

**Imetolewa na Baraza la Uongozi la Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS)**

**Boniface A.K Mwabukusi**
**Rais**